

**Taarifa ya Awali Kuhusu Tukio la Ujambazi lilitokea
Tarehe 28 Juni 2016 huko Rufiji - Mkoani Pwani**

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili mwaka 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya awali kuhusu tukio la ujambazi lilitokea tarehe 28 Juni 2016, saa 1.00 jioni huko Rufiji, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Juni 2016 majira ya saa 1:30 jioni katika Kijiji cha Nyamwege, Kata ya Mbwara, Wilaya ya Rufiji, watu wapatao watatu waliosadikika kuwa majambazi walivamia mabanda na magenge katika kijiji hicho na kupora simu za mkononi ambazo idadi na aina bado haijajulikana na kiasi cha pesa ambacho hakikufahamika mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tukio hilo, watu wawili waliuwawa ambao ni Ndugu Masoud Mayonga wa miaka 33 ambaye ni mfanyabishara wa Tigopesa ambapo alipigwa risasi ya kifuani na kufariki hapo hapo na mtu wa pili ni Ndugu Hamisi Njora, umri wa miaka 28, mfanyabiashara wa genge ambaye alishambuliwa kwa kukatwakatwa mapanga na kufariki dunia akipatiwa matibabu katika hospitali ya Misheni ya Mchukwi. Aidha, Ndugu Juma Said Ayoub wa umri wa miaka 25 mmiliki wa salon alijeruhiwa kwa kupigwa risasi ya mguu wa kushoto eneo la pajani wakati anajaribu kupiga kelele kuwaita majirani kutoa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa ya tukio hilo walifika eneo la tukio wakiongozwa na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Rufiji ambapo walikuta wahalifu hao walikuwa wametokomea kusikojulikana. Jeshi la Polisi limetuma Kikosi chake Maalum kutoka Makao Makuu ya Jeshi hilo kushirikiana na Makachero wa Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Rufiji kufanya msako mkali wa kuwakamata wahalifu wote waliohusika na tukio hilo. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Jeshi la Polisi liko imara na litawatia mikononi wahalifu wote waliohusika na tukio hili na kuwafikisha kwenye mkono wa sheria kama ambavyo wamekuwa wakifanya katika matukio mengine ya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Serikali kuwa wananchi wote wanaotegemea uhalifu kuendesha maisha yao waache mara moja kwani Serikali haitafumbia macho uhalifu na wahalifu wa aina yoyote ile. Aidha, nitoe rai kwa Watanzania kushirikiana na Jeshi la Polisi na kutoa taarifa mara moja wanapoona kuna dalili ama kuna watu wanaoonesha wanaweza wakawa na nia mbaya katika maeneo yao ili hatua ziweze kuchukuliwa za kuzuia uhalifu wa aina hiyo kabla haujatokea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa ulinzi na usalama wa nchi Kikatiba ni wa kila mwananchi. Kwa hiyo, naomba kutumia fursa hii kuwaasa Watanzania wote hususani wenye mapenzi mema na usalama wa nchi yetu kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ama vyombo vingine vya ulinzi na usalama pale wanapohisi au kusoma viashiria vya uhalifu katika maeneo yao ili hatua za haraka zichukuliwe kuweza kuzuia uhalifu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza katika kutoa taarifa hii. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*